


# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



## TAARIFA KWA UMMA

### UFAFANUZI KUHUSU ZOEZI LA UHAKIKI WA SIFA ZA WANAFUNZI WA VYUO VYA ELIMU YA JUU 2016/17

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kuarifu umma kuwa, uhakiki wa ubora wa wanafunzi wa elimu ya juu hufanyika kwa mujibu wa Kifungu 5(1)(b)(c) cha Sheria ya Vyuo Vikuu Sura ya 346 ya Sheria za Tanzania ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 42 ya Kanuni za Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2013.

Kama ilivyobainishwa hapo awali, hii ni mara ya kwanza uhakiki wa sifa za wanafunzi wa vyuo vyote nchini kufanyika kwa wakati mmoja.

Lengo la uhakiki lilikuwa kujiridhisha kuwa wanafunzi waliopo vyuoni ni wale waliodahiliwa kwa mujibu wa sheria na taratibu na kwamba wanakidhi vigezo stahiki. Uhakiki ulifanyika kwa kulinganisha taarifa zilizopo kwenye kanzi data ya Tume ya Vyuo Vikuu na zile zilizowasilishwa na Vyuo Vikuu. Uhakiki huo ulihusisha jumla ya wanafunzi 131,994 waliopo vyuoni kwa mwaka wa masomo 2016/17.

Baada ya kulinganisha taarifa zilizowasilishwa na vyuo na zile za TCU ilibainika kuwa asilimia 93.8 wana taarifa zinazooana na kanzi data ya Tume hivyo kuwa na sifa stahiki. Aidha asilimia 6.2 ya wanafunzi hao walikuwa na taarifa zilizokinzana na taarifa zilizopo katika kanzi data ya Tume.

Kufuatia hali hiyo, Tume ilitoa taarifa kwa umma kupitia tovuti ya Tume kuwaomba wanafunzi kutoa taarifa za ziada kupitia vyuo husika ifikapo tarehe

28 Februari 2017 ili kuharakisha kukamilisha uhakiki huo na kuweka kumbukumbu sahihi za mwanafunzi.

Hata hivyo imebainika kuwa taarifa hiyo imepokelewa kwa mtazamo na hisia tofauti na hivyo kusababisha mkanganyiko vyuoni. Umma unaarifiwa kwamba haikuwa nia wala lengo la Tume kusababisha mkanganyiko huo.

Kwa kuwa uhakiki wa sifa za wanafunzi ni kazi endelevu ya Tume na kutokana na maombi ya wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Kamati ya Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu na Wakuu wa Vyuo Vikuu Vishiriki Tanzania. Tume sasa itaendelea kuwasiliana moja kwa moja na vyuo katika kukamilisha zoezi hilo. Hivyo wanafunzi wote, wanaoendelea na masomo, waliokuwa wameorodheshwa katika taarifa iliyotolewa awali, wanaombwa kuwa watulivu na kuendelea na masomo yao kama kawaida ila wahakikishe taarifa zao ziko kamili.

Tume inapenda kuisitiza kuwa zoezi hili linahusu wanafunzi waliopo vyuoni tu ambao wanaendelea na masomo kwa mwaka huu wa masomo 2016/2017.

Aidha, ifahamike kuwa wanafunzi waliokuwa wameorodheshwa siyo kwamba wamethibitika kuwa hawana sifa stahiki, bali kuna mapungufu katika taarifa zao. Ndiyo sababu Tume iliwaomba kuthibitisha taarifa zao ili kuondoa mapungufu yaliyopo.

**Imetolewa na**  
**Kaimu Katibu Mtendaji**  
**1 Machi 2017**